# Vizimba 460 vyaanzishwa Ziwa Victoria

**Na Abela Msikula, Mwanza**

JUMLA ya vizimba 460 vya ufugaji samaki tayari vimeanzishwa katika Ziwa Victoria, huku Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ikiwahimiza wawekezaji kujitokeza zaidi kukamata fursa ili kukuza uchumi binafsi na wa nchi.

Mtendaji Mkuu wa Tafiri, Dk Ismael Kimirei, alibainisha hayo juzi katika mkutano wake uliowakutanisha wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi kujadili namna utafiti wa uvuvi na ufugaji samaki unavyoweza kuchangia uchumi wa bluu na ajenda ya ukuaji wa uchumi wa viwanda.

"Tafiti zinaendelea ili kubaini maeneo yote yanayofaa katika Ziwa Victoria kwa kilimo cha samaki wa vizimba. Tunatamani uwekezaji huu ufanyike katika vyanzo vyote vya maji nchini, ikiwemo Ziwa Tanganyika, Nyasa na Bahari ya Hindi," alisema.

Mbali na vizimba, Dk Kimirei alisema Tafiri pia imekuwa ikihimiza ufugaji wa samaki katika mabwawa ili kuongeza uzalishaji wa samaki nchini na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa jumla.

Alisisitiza wawekezaji kuwekeza katika sekta ya uvuvi na kuwahakikishia kwamba masoko ya samaki yapo ya kutosha nchini na duniani kote.

Alisema hivi karibuni Tafiri itaanzisha mfumo wa masoko wa kielektroniki ambao kila mzalishaji samaki atakuwa akitangaza biashara zake na bei husika kwa wateja wa ndani na nje ya nchi.

Akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk Rashid Tamatamah alikiri upungufu wa samaki katika vyanzo vya maji nchini kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, uvuvi haramu na uchafuzi wa mazingira ndani ya maji.

Kwa kulitambua hilo, serikali imeweka mipango ya kuongeza mchango wa sekta ya uvuvi, ikiwemo kupanua wigo wa uzalishaji wa samaki kutoka tani 497,000 za sasa hadi tani 600,000 kwa mwaka.

Scanned with CamScanner

# Nguvu zatakiwa kukomesha uvuvi haramu

**Na Suleiman Shagata, Mwanza**

HALMASHAURI zote mkoani Mwanza, zimetakiwa kuweka mikakati kuzuia uvuvi haramu unaoendelea na kutishia upatikanaji wa samaki katika Ziwa Victoria ili kuzuia tishio la kuisha kwa rasilimali hiyo muhimu kwa taifa.

Hayo yamebainishwa kwenye kikao cha watendaji wakuu wa serikali kutoka wilaya zote mkoani Mwanza kilichofanyika kupanga mikakati ya kufanya manunuzi kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo katika eneo hilo jana.

Mkurugenzi Idara ya Uvuvi, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Magese Emmanuel, alisema kuna haja ya kushiriki kwa halmashauri zote kwa nguvu kubwa kutokomeza uvuvi haramu unaofanywa kwa kutumia nyavu za timba.

Alisema kuendelea kwa uvunaji wa samaki ndani ya Ziwa Victoria kwa njia haramu unaathiri maendeleo na upatikanaji endelevu wa samaki, hivyo bila kuchukuliwa hatua kali za kimkakati kuutokomeza, upo hatari kwa samaki kuisha katika ziwa hilo.

Alisema yeye na watendaji wenzake kutoka wizarani wamekuja kusimamia utaratibu wa kutokomeza uvuvi huo haramu unaotishia kuangamiza rasilimali ya samaki katika Ziwa Victoria.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel aliwataka watendaji hao kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuelekeza njia za kitaalamu kwa watendaji wa halmashauri zote namna bora ya kutokomeza hali hiyo inayoweza kuhatarisha uwepo wa rasilimali hiyo muhimu kwa lishe bora kwa jamii.

Gabriel alisema serikali mkoani humo kwa pamoja itaongeza nguvu kubwa kuweza kutokomeza hali hiyo inayotishia upatikanaji wa samaki ndani ya ziwa Victoria.

Scanned with CamScanner